
# Ukaribu wa Mungu

## Ni Jambo la Thamani

## Jinsi gani Kujua Uwepo wa Bwana wangu



Gavin Devlin

# Ukaribu wa Mungu

## Ni Jambo la Thamani Jinsi gani Kujua Uwepo wa Bwana wangu

Gavin Devlin

fatheroflove.info

# Yaliyomo

Uhalisia wa Upatanisho kati ya Mungu Baba na Mwanadamu ........................ 4

Kioo .......................................................................................................... 7

Adamu na Hawa ........................................................................................ 9

Athari ya Anguko ...................................................................................... 10

Mungu huchukia kutengwa na wanawe ....................................................... 14

“Mwili ambao umeniandalia” – Mahali pengine pa kuishi pa Mungu ............ 18

Vitu najisi hututenganisha na Mungu .......................................................... 27

# Uhalisia wa Upatanisho kati ya Mungu Baba na Mwanadamu

Kabla nianze wacha tupige magoti kwa ajili ya ombi: Baba yetu mwingi wa neema, tunafurahia tena kuja mbele ya kiti chako cha enzi cha rehema na neema kupata msaada wakati huu wa hitaji. Kama kuna wakati ambao tunakuhitaji, ni sasa. Baba, tumetafuta ulimwenguni kote bila tumaini, lakini tunatazama Mbinguni kwa uhakika, kwa sababu tunajua unatawala, na kwamba ahadi zako zote zitatimia tukiendelea tu kukufuata, Bwana, na kukupa mioyo yetu. Nakushukuru kwa kutupa Yesu, mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu, na jinsi gani hutenda ndani yetu na kupitia kwetu kutenda mapenzi yako mazuri. Naomba kwamba unene kupitia kwangu. Nakushukuru kwa maandalizi ambayo yamefanywa katika kuweka haya pamoja, na Bwana, natazamia kuwabariki watu wako, wana wako, wakati huu. Kwa jina la Bwana Yesu, Amina.

Nataka kuchunguza uhalisia wa upatanisho kati ya Mungu na Mwanadamu. Upatanisho unamaanisha nini?

Umati: kuletwa pamoja tena.

Kuletwa pamoja tena! Unaweza patanishwa na usiletwe pamoja tena?

Umati: Hapana.

Haiwezi leta maana, sio? Kwa sababu sio kuunganishwa kama ndivyo. Na kwa hivyo mada yangu: “Ni Jambo la Thamani Jinsi gani Kujua Uwepo wa Bwana wangu” – hiyo ndio mada ndefu. Ni Jambo la Thamani Jinsi gani Kujua Uwepo wa Bwana wangu, au “Ukaribu wa Mungu” – hiyo ndio mada fupi.

Uumbaji – Mbona mtu aliumbwa? Mtu aliumbwa kwa mfano wa Mungu kwa kusudi: Mcheni Mungu na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imewadia. Mwabuduni Yeye aliyeziumba mbingu, dunia, bahari na chemchemi za maji. Ufunuo 14:7. Adamu na Hawa walikuwa na fadhila ya thamani sawa kama tulivyo leo. Waliubwa kwa ajili ya kazi hiyo ya thamani, kumtukuza Mungu, ambako ni kumuelewa na kuwakilisha tabia yake. Kazi

sawa tuliyonayo katika siku hizi za mwisho, ambayo ni kushiriki "Injili ya Milele," mpango wa Mungu kwa wanadamu ambao huonyesha jinsi alivyo. Kila kiumbe ambacho kiliumbwa, kiliubwa kumcha mungu, kuona uzuri wake, na kupokea wito wake, na kumtukuza katika maisha yao, na kumwabudu.

"Saa ya hukumu yake" iliwadia kwa sababu ya Lusifa kuasi mbinguni na kumuweka Mungu "katika uangalizi" kwa kuzua masuala fulani kumhusu ambayo hayakuwa ya kweli. Alifanya uongo na udanganyifu kumhusu Mungu, na theluthi ya malaika ilianguka katika udanganyifu wake (Ufunuo 12:4), na wakapoteza nafasi yao tukufu na ya kuheshimiwa mbinguni. Hata malaika waaminifu walichanganyikiwa na kusumbuliwa na tetesi za Shetani. Ikawa muhimu kwa Mungu kuondoa utata na kuelezea shauku ambayo viumbe walioubwa walikuwa nayo kwake kuhusiana na tabia yake na jinsi kanuni za utawala wake zinafanya kazi, hasa rehema yake na haki.

Ili kufanikisha hili, Mungu hakuita mkutano na kumlaani Lusifa na malaika walioasi mbele ya malaika wote waaminifu waliokuwa pale. Hakuzunguka akijaribu kuonyesha kuwa Lusifa alikuwa amekosea. Kitu kingine pia ambacho hakusema. "Msijali kuhusiana na kila kitu ambacho mmesikia. Niamini tu!" Hakuwa mwanabiashara.

Kukubali kipofu mapenzi ya Mungu hakungeleta mazingira ya upendo na ushirika ambayo Mungu alitaka, kwa sababu baada ya uongo wote na chongezi, baada ya ukweli wa kuhuzunisha wa vita vya maneno– malumbano, tetesi (Ufunuo 12:7) mbinguni – kulikuwa na uvunjaji wa uaminifu, udhabiti, na uimara ulimwenguni. Mungu alijua mahali ambapo shauku na vurugu zitafika, hata kama viumbe hawakujua.

Kwa hivyo katika hatua hiyo, kama Mungu angeinuka na kusema "Niamini tu," maneno yake yangekuwa mepesi na tupu. Shetani alikuwa hasa amemshtaki Mungu kama mbinafsi na asiye stahili kuaminiwa, na maneno hayakutosha kushinda madai hayo. Kuna kauli kwamba: "Ithibati ya mlo iko katika ulaji wake." Hivyo lazima uonje uone ya kuwa Bwana yu mwema (Zaburi 34:8). Lazima ulimwengu ungeonja na kuona.

Na hivyo ikawa, kama ilivyokuwa, thieta – lakini sio watu wakijifanya, sio watu wakiigiza, sio watu wakichukua majukumu. Mungu wala Mwanawe hawakuchukua majukumu. Sisi sio wakuchukua majukumu. Tuko katika vita halisi… na ni juu ya tabia ya Mungu na jinsi utawala wake hutenda kazi. Mungu hasa alikuwa akitazamwa na kuhukumiwa kuhusiana na jinsi angekabiliana na matatizo yaliyosababishwa na uasi wa Lusifa.

Kilichohitajika kilikuwa ni *onyesho* hili la kazi ya kanuni ya ufalme wa Mungu. Na kwa hivyo Mungu, hata ingawa tayari alikuwa na mpango wa kuumba mwanadamu, kufanyisha kazi mpango huu baada ya anguko la Lusifa. Ilikuwa kupitia kwa kutazama kilichofanyika katika ulimwengu huu, kupitia kwa kuongezeka kwa familia ya mwanadamu, ufalme wa Mungu ungekuwa wazi.

Kwa hivyo Mungu aliumba wachumba hawa, kwa sura yake. "Kwa mfano wa Mungu aliwaumba" mwanaume na mwanamke: mwanaume kichwa cha nyumba, na mwanamke msaidizi, naibu. Kama vile Baba alivyo kichwa cha Kristo, na Kristo humsaidia Baba yake kwa vitu vyote, ndivyo Hawa alikuwa amsaidie mume wake katika kutawala vitu vya dunia. Katika utawala wao kwa vitu vya duniani, juu ya viumbe vya sayari na kuwakuza wanao, wataonyesha kupitia kwa utiifu wao na uaminifu kwa Mungu jinsi Mungu alivyokuwa, na jinsi utawala wake hutenda kazi.

Baada ya kumuumba Adamu kutoka kwa mavumbi ya nchi, Mungu alimpulizia puani mwake pumzi ya uhai, na Adamu akawa nafsi hai. Katika kupokea Roho wa Mungu, Adamu alipokea uwezo wa kuimarisha, karama ya uzima … alianza kupumua na akafungua macho yake na akatazama juu na akamuona muumbaji wake. Huo lazima ulikuwa wakati wa kupendeza kwa Adamu.

Lakini haikutosha kwa Adamu kuishi tu na kupumua! Mungu alitaka uhusiano wa kina na Adamu, na kwa hivyo pamoja na uwezo wa kuimarisha uzima alipewa uwepo wa Mungu, ambao pia ulijaza Adamu na Hawa. Udhihirisho wa uhalisia huo wa ndani ulikuwa mwanga wa nje wa kupendeza, vazi la mwanga ambalo lilionyesha kwamba uwepo wa Mungu ulikuwa ndani yao na pamoja nao.

Bibilia inatwambia kwamba walikuwa uchi lakini hawakuona aibu. Hawakuwa na sababu ya kuaibika kwa sababu walifunikwa kikamilifu, kama Mungu alivyowaumba, kwa mwanga huu wa kupendeza. Mwanga ulikuwa sawa kabisa na ule ambao Musa alikuwa nao alipokaa mlimani kwa siku arobaini na Mungu. Aliposhuka kutoka mlimani uso wake uling'aa, na kwa hivyo aliombwa kuweka kitu kwa uso wake ili kufunika utukufu. Uling'aa sana kiasi kwamba watu hawangeutazama. Yesu pia alikuwa na Mwanga huu alipoenda kwenye mlima wa uhamisho wa sura yake pamoja na wanafunzi wake. Musa na Eliya walishuka, na Baba alinena wakati huo – "huyu ni Mwanangu mpendwa: msikilize," na tena kulikuwa na mwanga huo wa utukufu juu ya Kristo. Hivi ndivyo Adamu na Hawa walivikwa kiasilia.

## Kioo

Kama vile Adamu na Mkewe waliakisi utukufu wa Muumbaji na Mwanawe, ndivyo pia maumbile yalikuwa yaakisi uhusiano huo wa kupendeza kati ya Adamu na Hawa, na kati yao na Mungu. Kama mwanadamu alivyo nyenyekea kwa Mungu n a kutii mapenzi ya Muumbaji wake, akikuza na kushiriki ufahamu wa tabia na njia yake, ndivyo maumbile yangenyenyekea kwa mwanadamu na bustani ingekuza uzuri wake na mazao yake katika hili, tabia ya Mungu na kanuni za utawala wake zingeonekana kwa uzuru zaidi, na kuwasilishwa kikamilifu.

Kwa bahati mbaya, kama sote tujuavyo vyema, sio kila kitu tunachopanga hutokea tulivyopanga. Na kama ilivyo kwetu, ndivyo ilivyo kwa Mungu. Sio kila kitu katika mpango wa Mungu kimetimia alivyopanga.

Wakati ambao watu au malaika wamepewa karama ya thamani mno ya uhuru wa kuchagua, daima kuna fursa ya mtu kuchagua kusema "Hapana, sitaki kufanya namna hiyo, nataka kufanya kwa namna yangu!"

Kwa hivyo, kuna baadhi ya kanuni za tabia ya Mungu na utawala ambazo hutumiwa, iwe ni wakati wa uzuri au wakati wa mabaya.

Kanuni 1 – Mungu amekipa kila kiumbe chenye maadili karama ya uhuru wa kuchagua … kila mmoja!

Kanuni 2 – Mungu kamwe hatatengua karama hiyo, hata athari iwe namna gani … nzuri au mbaya.

Kanuni 3 – Mungu yuko tayari kujivika athari ya uchaguzi wetu mbaya… Hivyo tunapaswa kuwa tayari kubeba athari za uchaguzi wetu mbaya, lakini hapo sio tulipo!

Kanuni 4 – Mungu atafanya kila awezacho ili kutukomboa kutoka kwa uchaguzi wetu mbaya, kutuonya kwa kujaribu kutuokoa. Kitu pekee ambacho hawezi fanya ili kutuokoa kutoka kwa uchaguzi wetu mbaya ni kutulazimisha. KAMWE hatatumia nguvu.

Kanuni 5 – Mungu atatuacha tuteseke kwa ajili ya athari za uchaguzi wetu mbaya haijalishi ni makali namna gani tutakapokataa msaada wake wa kutusaidia na kutukomboa. Kwa sababu ya kujitolea kwake kwa uchaguzi huru, hawezi ingilia kati katika maisha yetu bila kukaribishwa. Habari njema ni kwamba tunaweza omba kwa niaba ya wengine. Kama wanadamu wenzao tunaweza mkaribisha Mungu kuingilia kati, hivyo kuna jukumu kuu kwetu kutenda!

Kanuni 6 – Mungu yuko tayari kuwajibikia kikamilifu matokeo ya mambo yote chini ya utawala wake huru kwa sababu huruhusu yatendeke. Anaweza sema "Hapana, sitaruhusu jambo hilo litendeke, sitaruhusu uwe na uhuru huo wa uchaguzi. Siwezi ruhusu hilo, kwa sababu karibu unafanya uamuzi mbaya!" Mungu hafanyi hivyo. Huwajibikia kikamilifu matokeo, hata kama humaanisha mauti yetu. Hutupa uhuru wa kwenda upande huo kwa sababu ya kanuni za kwanza 5.

Kanuni 7 – Mungu kama Muumbaji wetu, anahuzunika tunapogeuka kutoka kwake, na anateseka katika mateso yetu yote (Isaya 63:9). Pia anafurahia kwa nyimbo tunaporejea kwake. Kwa hivyo, anatufahamu kwa karibu sana. Na ndio maana hufanya kila awezalo kutuonya kabla ya kufanya maamuzi yetu mabaya. Ameahidi kufanya kila awezalo kutuokoa tunapofanya uchaguzi

mbaya na kufuata njia mbaya. Yuko na mfundo wa uokozi, mfundo mkuu wa uokozi kuwahi wekwa mahali pake! Na anahamu ya kuturejesha kwa uhusiano wetu wa asili naye kwa kutuonyesha upendo wake: kanuni za msingi na nguzo za tabia yake na utawala wake! Sio rahisi kwetu kufahamu upendo wake, kwa hivyo Mungu amekuwa akionyesha utawala wake wa upendo kwa miaka 6000 iliyopita, akisubiri siku ambayo yote yataingia mahali pake na wanadamu watakuwa na wakati wa 'eureka' na Yesu ataweza kurejea!

## Adamu na Hawa

Tunaingia katika kisa cha Adamu na Hawa katika bustani. Tunajua matokea. Nyoka aliwajaribu, aliwadanganya na kuwafanya kuanguka kupitia kwa mapenzi yao wenyewe ya kukataa neno la Mungu na badala yake kupokea maneno ya nyoka. Walitumia uhuru wao kuchagua kuishi namna nyingine kando na ile ambayo Mungu alikuwa amewaelekeza. Hili lilipelekea utukufu wa Mungu kuondoka kwao. Vazi la mwanga ambalo walikuwa wameumbwa nalo, hawakulimiliki tena, na sasa walitambua uchi wao.

Gundua kwamba kanuni, ambazo nilitaja awali, katika kisa hiki.

Kanuni 1: Walitumia karama ya uhuru wao wa kuchagua kuchukua na kula tunda walilokatazwa.

Kanuni 2: Mungu hakutengua uhuru wao na kuchagua kwa niaba yao katika majaribu.

Kanuni 3: Mungu alikuwa tayari kubeba athari za kukataliwa kwa uchungu ambao ingemsababishia, na uchungu ambao ingewasababishia.

Kanuni 4: Alidhihirisha mpango wake wa kuwakomboa. Habari njema! Mungu hatuache pweke. Kamwe hawezi kubali kukataliwa bila kujaribu kurejesha upendo wetu kwake. Hufanya kila awezacho kurejesha uhusiano huo nasi, ili tuweze kuunganishwa naye tena.

Kanuni 5: Athari za uchaguzi wao zilijitokeza wazi kwao wakati ambao vazi lao la utukufu wa mwanga lilififia na kuondolewa katika makazi yao ya bustani.

Kanuni 6: Akijua kile athari ya dhambi yao ingeleta kwa wana-ndoa, mungu bado aliruhusu wajifunze katika bustani hiyo kubwa ya maisha, nje ya Bustani ya Edeni. Ulimwengu huu ukawa thieta na darasa la maisha. Hapa ndipo maumbile yalikuwa yaakisi kilichokuwa ndani ya Adamu na Hawa na familia yao. Moyo wa mwanadamu ni chombo ambacho huongoza viwango vya msongo na faraja vya maisha. Maumbile ni kipimajoto ambacho hudhihirisha viwango viko wapi. Tambua kwamba moyo wa mwanadamu hauonekani na maumbile yanaonekana. Wakiendelea na maisha yao mengine, wangejifunza hali ya mioyo yao, na athari ya dhambi yao, kupitia kwa uakisi wanaopokea kupitia kwa maumbile. Hili hutokea sawasawa katika wakati wetu wa sasa. Miiba ilikuwa udhihirisho wa uasi wa Adamu na Hawa, kama tu machafuko ya mazingira leo ni udhihirisho wa machafuko na vurugu katika mioyo ya wanadamu. Swali – Ni nini maumbile yatatwambia kabla tutambue hali yetu ya kuvunjika?

Jambo lingine ambalo ni muhimu kukumbuka ni uchungu ambao Mungu anahisi kwa sababu ya anguko la mwanadamu. Kutengwa kutoka kwa wanawe humsababishia Mungu uchungu usio na mwisho. Kuwafikia na kukataliwa wakati wote, akijua kwamba kukataliwa huko kuna athari ya mauti, humjaza Kristo maumivu. Sio rahisi kwa Mungu kuona wanawe lazima watembee katika ulimwengu wetu wa mateso na uchungu. Kila mwiba na mchongoma, unaoshuhudiwa na mwanadamu, ni kioo kinachoonekana cha uchungu ambao Baba yetu wa mbinguni pia anateseka, anapotengwa kutoka kwa wapendwa wake.

## Athari ya Anguko

### **Athari nambari ya 1**: Hukumu na Adhabu

Adamu na Hawa waliposikia sauti ya BWANA MUNGU akitembea kwenye bustani, hisia zao za kujihukumu nafsi ziliwafanya Adamu na Hawa kukimbia na kujificha miongoni mwa miti. Hakuna rekodi yoyote ya hukumu yoyote

ikitoka kwa Mungu. Mungu anauliza tu mfululizo wa maswali kujaribu na kuwafanya Adamu na Hawa kufikiria kuhusu uchaguzi wao na jinsi walivyokuwa wakihisi wakati huo – jinsi walivyokuwa wakihisi kumhusu, na jinsi walivyokuwa wakihisi kujihusu.

Katika Warumi sura 5, fungu 15 hadi 17, Paulo anachukua hoja hii. Nimeonyesha kile ambacho adamu alitenda kwa rangi nyekundu, na kile ambacho Mungu ametenda, kupitia kwa Kristo, kwa rangi ya samawati. Ni mizani tu - Adamu na Kristo; Adamu, Kristo; Nyekundu, samawati. Hivyo tunaweza shika, katika mtiririko huu, hasa ni nani mshtaki, nani hakimu. Mungu ndiye hakimu? Mungu ndiye mshtaki? Au Adamu ndiye Hakimu? Adamu ndiye Mshtaki? Kwa hivyo tazama mizani inavyoenda [kwenda na kurudi]:

Katika Warumi 5:15

"Lakini ile karama iliyotolewa haikuwa kama lile kosa (Kupitia kwa Adamu) Kwa maana ikiwa watu wengi walikufa kwa sababu ya kosa la mtu mmoja, zaidi sana neema ya Mungu na ile karama iliyokuja kwa neema ya mtu mmoja, yaani, Yesu Kristo, imezidi kuwa nyingi kwa ajili ya wengi."

Fungu 16

"Tena, ile karama ya Mungu si kama matokeo ya ile dhambi. Hukumu ilikuja kwa njia ya mtu mmoja ikaleta adhabu, bali karama ya neema ya Mungu ilikuja kwa njia ya makosa mengi, ikaleta kuhesabiwa haki (Kristo)."

Fungu 17

"Kwa maana ikiwa kutokana na kosa la mtu mmoja, mauti ilitawala kupitia huyo mtu mmoja (Adamu), zaidi sana wale wanaopokea wingi wa neema ya Mungu na karama Yake ya kuhesabiwa haki, watatawala katika uzima kwa njia ya huyo mtu mmoja, yaani, Yesu Kristo.

Tazama usawazishaji huo wa kupendeza kwote! Itakuwa kufurukuta kwa maandiko kusema kwamba Mungu alikuwa hakimu kwa nuru ambayo ya jinsi Paulo ameielezea hapa … Adamu … Kristo, Adamu … Kristo. Hukumu na Adhabu ilitoka kwa ADAMu … **haikutoka kwa Mungu!**

Ilikuwa hukumu ya nafsi yao wenyewe ambayo ilichochea kutosita kwao kukimbia na kujificha walipoitwa na Mungu – na sisi hatuku hivyo pia? Ni mara ngapi katika maisha yetu, kama ni mambo ya kidini au hali nyingine katika maisha, sisi ndio ambao tunakimbia na kujificha mtu fulani au jambo fulani kwa sababu ya jambo ambalo tulifanya? Ilikuwa hukumu ya nafsi ya Adamu na Hawa ndio ilichochea hamu yao ya kukimbia na kujificha, kwa hivyo kuanzisha utengo, ambao dhambi ilisababisha, kati yao na Mungu. Ni huku ya nafsi yetu wenyewe ambayo pia husababisha tukimbie, na kusababisha kutengwa kutoka kwa Mungu.

## **Athari Nambari ya 2**: <u>Utengo</u>

Isaya 59, Fungu 1:
"Tazama, mkono wa Bwana haukupunguka, hata usiweze kuokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia."

Mkono wa Mungu sio haujapungua ati asitusaidie tena. Na hahitaji kusikia!

Lakini fungu la 2 linasema:
"lakini maovu **yenu** yamewafarikisha **ninyi** na Mungu wenu, na dhambi **zenu** zimeuficha uso wake msiuone, <u>hata hataki kusikia</u>."

Tazama, Mungu hatatusikia! Lakini waza kuhusu hili. Mbona asitusikie? Anawaona Adamu na Hawa katika bustani, kwa hivyo mbona hakusikia? Ni kwa sababu walikuwa wamekimbia na kujificha kutoka kwake! Walikuwa wameacha kuzungumza naye. Hakuna wakati ambao unaweza msikia mtu ambaye ameacha kuzungumza nawe… kweli? Sikio la Mungu sio ziti hata asiweze kusikia! Lakini hawezi sikia wakati ambao hauzungumzi naye.

Umati: Pengine uwe unazungumza na mungu ambaye siye.

Ndio, hilo linaweza kuwa tatizo pia!

Umati: unaweza kuwa unazungumza na upepo.

Ni utengo wetu ambao hutoka katika hukumu ya nafsi zetu wenyewe, kukimbia na kujificha kutoka kwa Mungu, humfanya Mungu asiwezi kutusikia.

**Athari Nambari ya 3**: Mauti

Mara tunapojihukumu, kujiadhibu, na kukimbia kutoka kwa Chemchemi ya Uzima … tokeo dhahiri ambalo litakuwa daima ni lipi?

Umati: Mauti.

Mauti! Kujitenga kutoka kwa Chemchemi ya uzima ni mauti! Sio adhabu ya kiholela kutoka kwa Mungu. Kamwe haikuwa na daima haitakuwa!

# Mungu huchukia kutengwa na wanawe

Mapenzi ya Mungu ni kuwa karibu na wanawe **…** Daima! Mapenzi yake hayajawahi badilika. Inaonyeshwa wazi katika Mwanzo 3 kwamba dhambi haitengi Mungu kutoka kwetu. Hututenga *sisi kutoka kwa Mungu*. Sisi ndio ambao hukimbia! Mungu hana shida na sisi. Tuna shida na Mungu!

Ukweli hasa kwamba Mungu alikuja kwenye bustani kuwatafuta wanawe unatuonyesha wazi jinsi Mungu anawapenda. Inaonyesha pia jinsi anatupenda! Mapenzi yake ya kuwa nao hayakuwa yamedidimia kwa njia yoyote ile, kama vile mapenzi yake yakuwa nasi hayajididimia kwa njia yoyote ile, umbo au namna. Sababu ambayo Mungu hawezi tukaribia katika hali yetu ya dhambi sio kwa sababu hataki kuwa karibu nasi … sio kwa sababu hataki kuwa nasi! Ni kwa sababu hatutaki kuwa karibu naye. Hatutaki kuwa naye! Mwanga wa utukufu wake na utakatifu wa tabia yake utakuwa kwetu moto ulao wa kujihukumu nafsi na kusababisha kifo cha papo hapo … na hili Mungu ataepuka kwa vyovyote vile.

Sio jambo la kupendeza? Isn't that amazing? Jambo la ajabu! Upendo wa Mungu kwetu ni mkuu sana. Tukijua kwamba wema wake ni wenye nguvu zaidi, hawezi hata akadhihirisha ukamilifu wa utukufu wake kwetu ili usitutawanye na kutuua: na kwa hivyo amejidhihirisha taratibu, kwa kiasi, polepole akifanya upya uhusiano wake nasi.

Tunajua kwamba mawasiliano yote kutoka Mbinguni ni kupitia kwa Mwana wa Mungu. Mungu, Baba yetu, kamwe hazungumzi mwenyewe nasi. Huzungumza kupitia kwa Mwanawe. Hata Roho wake hutiririka kupitia kwa Mwanawe! Mungu anapotaka kuzungumza nasi, huzungumza kupitia kwa mwakilishi wake, Kristo. Kristo ndiye mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu (1 Timotheo 2:5).

Kadri muda ulivyosonga, utengano kati ya Mungu na wanawe ulizidi kuimarika zaidi na zaidi. Kuwa mbali na mwana mmoja ni kwa kuvunja moyo kwa Mungu. Tafakari wanao wote wakikutupilia mbali wakati ambao unataka kuwa nao sana. Mtazamo wa upendo wake wa Agape kwa kila mwana binafsi

au wanawe wa kwanza wawili Edeni ni na ulikuwa mkuu zaidi kiasi kwamba kukataliwa ni na kulikuwa kama kifo kwake na kwa Mwanawe. Kukataliwa kulichoma mioyo yao siamini tunaelewa. Kristo ndiye Mwana-kondoo aliyeuawa tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu kwa sababu ya utengano uliosababishwa na dhambi. Anashiriki uchungu wa Baba yake. Mungu anatamani kuwa karibu nasi na kutuona tukiishi kwa furaha na utimilifu.

Kumekuwa na baadhi ya wale ambao walimruhusu Mungu kuja karibu nao katika utu wa Mwanawe. Kumbuka Enoko … Enoko alitembea na Mungu. Yeye na Mungu walikuwa karibu kiasi kwamba alitembea hadi mbinguni naye … akirejea kwa nyumba ya Baba yake.

Nuhu alipata neema machoni pa Bwana. Na ninauhakika kwamba maandiko hayaelezei visa vyote vya watu wote ambao walikuwa na uhusiano wa kupendeza Mungu kabla ya gharika. Baada ya gharika kulikuwa na Abrahamu, ingawaje Abrahamu alikosea. Abrahamu alikosea?

Umati: ndio.

Ila Abrahamu aliitwa "Rafiki wa Mungu." Hili lazima liliathir wanawe na uhusiano wao na Mungu. Isaka, Yakobo na Yusufu wote walikuwa na uhusiano mzuri na Mungu ingawa walikuwa na changamoto zao. Wote walishikilia kwa imani ahadi za Mungu. Vizuri! Lazima walikuwa wamepatanishwa!

Kwa bahati mbaya lakini, wengi wa wana wa Mungu wenye balaa hawakuwa, na kimsingi hawakutaka kuwa na uhusiano na baba yao wa mbinguni kwa sababu mbalimbali; na hilo linaendelea kumuumiza Mungu zaidi ya uwezo wetu wa kufahamu.

Kumbuka hisia wakati umehisi vibaya kabisa … wakati ambao umekataliwa na mtu. Hila huhuzunisha! Wakati mmoja nimewahi elezea kisa change kuhusu kumwaga machozi katika kampuni ambayo nilifanya kazi kwa muda mrefu. Alikuwa Mkristo mwenzangu. Ambaye alinihuzunisha! Na nilibeba hilo kwa muda mrefu!

Fikiria uchungu ambao Baba yetu amekuwa akibeba kwa muda mrefu zaidi! Mungu angefanya nini wakati ambao watoto wake walizidi kumsukuma mbali, bila kutaka kumjua?

Vyema, aliwaongoza wana wa Israeli kutoka Misri, akiweka huru kutoka mateka na utumwa ambao walikuwa ndani kwa karne nyingi, Alimwambia Musa, kama ilivyorekodiwa katika Kutoka 25:8, "Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao." Mungu alijua kwamba Waisraeli, kwa kuwa mateka kwa muda mrefu, walihitaji wasilisho linaloonekana la uwepo wake ili waweze kuamini kwamba alikuwa karibu nao. Kupitia kwa mfumo wa Patakatifu wangepata ufahamu wake, na kwa hivyo kuwavuta karibu.

Nitaonyesha kidogo tu jinsi bila shaka ingeonekana. [Anachora mstatili mdogo kwenye ubao mweupe kuwakilisha patakatifu na kandokando ya mviringo huo akiwakilisha kama watu milioni wa Israeli]

Katikati ya Waisraeli kuna Patakatifu … na katika Patakatifu, kulikuwa na chumba kingine kidogo, Hema ya Patakatifu … na katika Hema ya Patakatifu, kulikuwa na kichumba kidogo zaidi, patakatifu, na nyuma ya pazia patakatifu pa patakatifu palikuweko … bado mnaona picha? Mnaona maelezo ya sanduku la Agano ambalo nimechora? [Kicheko] sawa! Hapo ndipo Mungu anakaa! Utukufu wake ulikaa juu ya sanduku la agano: miongoni mwa wana wa Israeli walipoweka kambi wakizunguka jangwani.

Walipotoka Misri Mungu alijiwasilisha kwao kwa wingu mchana na kwa nguzo ya moto usiku, lakini bado, alitaka kuwa karibu zaidi nao. Alitaka kuwa chini pamoja nao. Wana wa Israeli walitoa vitu ambavyo vilihitajika, na wakajenga Patakatifu. Mungu alipanga mahali padogo pa kipekee ambapo atakaa nao katika sehemu hiyo ndogo. Sanduku la ushuhuda wake lilikuwa pale, likiwakilisha enzi yake ya milele, na alipokuja kuwa nao, hapa palikuwa pahali pake.

Lakini kwa kweli, tunafikiria kwa dakika moja kwamba Mungu angeridhika kukaa tu katika kichumba kidogo na kuzuiliwa kwa pahli pake padogo pa kuwa karibu na wanawe? Hapana! Hiyo haikutosha. Haikutosha kwake na bila

shaka haikutosha kwa wana Israeli kujifunza kumhusu. Waliendelea, kama Adamu, kutomuelewa Mungu, na kumfikiria kuwa kitu tofauti mbali na kile ambacho alikuwa kweli. Walidhani kwamba kujiweka kwake tu katika Patakatifu pa Patakatifu lilikuwa jambo la ajabu … pengine hivyo ndovyo walifikiria … haijaandikwa kwenye maandiko. Lakini mbona Mungu anajificha katika Patakatifu, katika Hema, katika Patakatifu pa Patakatifu juu ya sanduku na hakuna hata mmoja wenu anamuona? Isipokuwa walipokuwa wakisafiri, katika wingu mchana, na nguzo la moto usiku.

Haikutosha. Tumesikia mahubiri mengi kuhusu kukanganyikiwa huku kumhusu Mungu ambako sisi kama wanadamu tunakwo, na haikuwa tofauti kwao wakati huo. Walifikiria kuwa Mungualikuwa hakimu mkuu, mshtaki mkuu wa wale ambao walipungukiwa na utukufu wake: hasaa adui zake huko nje. Bila shaka lazima awachukie wote! Kwa hivyo hawakupata picha … hawakupata ufahamu.

Na kwa hivyo funzo ambalo Mungu alipanga lisomwe kupitia kwa Patakatifu na Huduma yake halikusomwa na Waisraeli. Kwa kweli, ilikuwa vibaya zaidi kwamba wana wa Israeli waliiendea miungu mingine kwa sababu iliguzika zaidi na bila shaka rahisi kutuliza.

Mungu alihitaji kutulizwa? Alitaka hilo kwa njia yoyote ile? Hapana! Mungu alitaka tu kujulikana na wanawe mwenyewe, na hii ilidhihirisha kuwa kazi ngumu kutekeleza. Mungu alijua njia pekee watu wangemjua jinsi alivyo kwa kweli, ilikuwa kuwasilishwa kisahihi kwa kitu ambacho wangeona. Pengine mwanadamu mwenzao? Kwa hivyo hili alifanya kupitia kwa Mwanawe.

Tunatoka kwa Patakatifu hadi kwa Mwana wa Mungu.

## “Mwili ambao umeniandalia” –
## Mahali pengine pa kuishi pa Mungu

Mungu alimtuma Mwanawe kiumbe pekee ulimwenguni aliyemjua kwa karibu na kikamilifu na angeweza kumuwakilisha jinsi alivyo kweli. Amina?

Umati: Amina!

Halleluya kwa hilo!

Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee ili kumuwakilisha. Yesu alikuja na akasema kwa msisitizo, “Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba. Maneno ninayowaambia siyasemi kwa ajili Yangu mwenyewe, bali Baba akaaye ndani Yangu ndiye atendaye hizi kazi.” (Yohana 14:9-10)

Kwa hivyo kama tunataka kujua jinsi Mungu alivyo… na tunataka na tunahitaji kujua jinsi Mungu alivyo… basi ushahidi A … ni Yesu! Kwa vile hili hakika halikutendeka (akiashiria picha ya patakatifu kwenye ubao mweupe) … haikutosha kwao au sisi, ingawa kuna mafunzo kutoka kwayo ambayo bado tena tunaweza pata nuru kutoka kwayo.

Waebrania 10:5

“Kwa hiyo, Kristo alipokuja duniani alisema,

“Dhabihu na sadaka hukuzitaka,

bali mwili uliniandalia.’

Yesu alipokuja haikuwa kwa lengo la kufa. Watu hudhani kwamba Mungu huhitaji damu ili kutusamehe. Lakini hicho sio kile kilikuwa!

““DHABIHU NA SADAKA HUKUZITAKA, BALI MWILI ULINIANDALIA” … mwili? Wa kusulubiwa tu? La, la, la, la! Mwili ambao kwao atawasilisha tabia ya baba yake… vizuri … kwa watu wanaomzunguka.

Tazama jinsi vazi hili linasema wazi kuhusu suala hili! Haikuwa **kumtuliza** Mungu, ilikuwa **kumwakilisha** Mungu ili kwamba tuweze mjua: na Yesu alifanya hili katika mwili.

Yohana 1:14

"Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi takauona utukufu Wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli."

Bila shaka tunajua hadi mwisho wa kazi yake, alipokuwa akiomba kwa Baba, Yesu alisema, "Nimekutukuza Wewe duniani: **Nimeitimiza** ile kazi uliyonipa niifanye" (Yohana 17). Kazi hii ilikuwa kudhihirisha kwa watu jinsi Mungu alikuwa kweli: na Yesu alifanya hilo kikamilifu. Lakini kulikuwa na zaidi kwayo kuliko hilo. Kumbuka Mungu alitaka kuwa karibu na wanawe, na ilikuwa kupitia kwa Kristo, au niseme **Katika** Kristo, kwamba Mungu Baba aliweza kuchukua hatua nyingine karibu na kuwa na wanawe.

Sawa … Hapa kuna Yesu (akichora kwenye ubao mweupe picha ya Yesu). Kwa hivyo Yesu yuko hapo … Mungu yuko wapi? Awali Mungu alikuwa na pahali padogo juu ya sanduku katika Patakatifu. Sasa Mungu alikuwa na pahali **NDAN**I ya Mwanawe. "Kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake mwenyewe."

Sanduka halikusongezwa isipokuwa walipokuwa wakisafiri, na Shekinah bila shaka haikuwa pale wakati ambao sanduku lilikuwa linabebwa. Lakini sasa Mungu alikuwa na Mwanawe wa kuweka wazi tabia yake, kuongezea uzito kwa yale alikuwa anajaribu kusema katika mfumo wa patakatifu. Yesu alikuwa nje na tayari, kuchanganyika na watu, na Baba aliweza kuchanganyika na wengi wa wanawe zaidi kupitia kwa Kristo. Unaona hatua kutoka mahali hapa pa kudumu (Hema), kuweka ambapo anaweza ondoka na kuwa karibu kupitia kwa Mwanawe?

2 Wakorintho 5:18

"Haya **yote** yanatokana na Mungu, ambaye ametupatanisha sisi na nafsi yake kwa njia ya Yesu Kristo na kutupatia sisi huduma ya upatanisho"

Hiyo ni hatua inayofuata …

## Fungu 19

“Kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake mwenyewe, akiwa hawahesabii watu dhambi zao. Naye ametukabidhi sisi ujumbe huu wa upatanisho.”

Zingatia kwa ukaribu: upatanisho kati yetu na Mungu haukutegemea mfumo wa *kutuliza*. Haingeweza kwa sababu utulizo haudhihirishi kisahihi *tabia* ya Mungu. Hukumu ilitoka kwa nani? Kwa Adamu, sio kutoka kwa Mungu. Kumbuka Warumi 5:16.

Utengano ulitoka kwa Adamu, sio kwa Mungu. Adamu alikimbia na akajificha, sio Mungu. Mungu alijua kilichokuwa moyoni mwa Adamu. Adamu hakujua kilichokuwa moyoni mwa Mungu. Alikuwa amepofushwa na adui ambaye alikuwa amefurukuta mawazo yake kwa habari bandia kumhusu Mungu. Alimeza ndoano, mfululizo na kizamishi!

Kutoelewa kulikuwa tatizo la Adamu, sio la Mungu. Kwa hivyo, suluhisho la kutukomboa kutoka kwa dhambi haikuwa kuleta hofyu zaidi na hukumu kupitia kwa mfumo wa kutuliza na kafara, mbali kuleta amani na thibitisho kwa Mungu anatupenda – na kwamba upendo kwetu haujawahi didimia – na hili alilitenda kupitia kwa mwili ambao aliandaa … Mwanawe.

Mwakilishi halisi wa wema wa Mungu katika utukufu wake wote alikuwa atolewe ili mawazo ya wanadamu yatulie. Kutulia ndiko kulikuwa muhimu, **sio** kutuliza. Tulihitaji mioyo yetu itulizwe, kuwa katika utulivu na Mungu – kuona jinsi alikuwa kwa kweli katika upendo wake WOTE. Kuona tu upendo wa Mungu wa kweli kwetu kunaweza vuta mioyo yetu kwa Mungu tena. Huu ni upatanisho! Hili lilifanywa vyema na kikamilifu zaidi katika na kupitia maisha ya Bwana wetu, Mkombozi wetu na Ndugu Mpendwa, Yesu Kristo.

<u>Maisha ya Yesu</u> yanaonyesha wazi *jinsi <u>Mungu</u> alivyo*. <u>Kifo cha Yesu</u> yanaonyesha wazi *jinsi <u>sisi</u> tulivyo*. Mungu ni mpaji wa uzima na hakuna lingine zaidi. Sisi kihalisia ni wauaji na hakuna lingine zaidi. Mungu anaishi katika matumaini. Tunaishi kwa hofu. Mungu hufurahia kwa rehema.

Tunafurahia katika hukumu: ndio maana tunaishi kwa hofu. Tunavyohukumu ndivyo tunatarajia kuhukumiwa. Kumbuka kisa cha Kaini.

Tunatarajia Mungu atuhukumu kwa sababu ndivyo tufanyavyo; tunadhani ya kuwa Mungu ni kama sisi (Zaburi 50:21). Watu wengi hufikiria kwa njia hiyo, kuhukumu na adhabu kila wakati. Hivyo ndivyo watu wengi huishi, na kuendelea, na kutenda, na kuwa na utu wa haswa, wakidhani kwamba Mungu anawahukumu na kuwaathibu na kuwaangamiza kila wakati, wakati ambao kihalisia tunaishi katika kivuli cha sanamu ya ufahamu wetu potovu. Na hili huleta kujihukumu nafsi na kuwahukumu wengine: mechi ya kupakana ambayo haiishi kwamwe.

Ili kuvunja mviringo wa kujihukumu nafsi na hofu ya Mungu, Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee, Yesu, kuonyesha tabia yake ya rehema, wema wake wa *milele* na neema yake tukufu zaidi. Hatuhitaji kumhofu Mungu tena: sura ya Mungu imerekebishwa. Ufahamu sio na potovu umeondolewa: na kwa hivyo mchakato wa upatanisho umekamilishwa katika Kristo. Tunapofahamu kwamba mawazo ya Mungu kwetu ni amani, na tumaini, na wingi wa furaha, tutampokea kwa unyenyekevu kamili wa maisha yetu kwa mipango yake. Tutampa mioyo yetu kwa utunzaji salama, lakini wakati ambao tu tumepatanishwa mioyoni mwetu kwa kweli. Hiyo ndio maana Yesu Kristo ni mwanzilishi na mkamilishaji wa Imani … ndio maana ni Mwanzilishiji na Mkamilishaji wa Imani *yetu*. Kwa sababu ni kupitia kwa kumtazama tunamfahamu Mungu na kutambua, hatimaye, kiwango ambacho anatupenda.

Halleluya, kwa sababu maelezo ambayo Mungu alimpa Musa kujihusu miaka hiyo iliyopita kuhusu tabia yake yalithibitishwa kuwa sahihi. Kweli? Unaamini hivyo? Katika Kristo yamethibitishwa kuwa sahihi! Mungu ni “Mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi.” (Kutoka 34:6,7). Hiyo ndio hisia ya Mungu kwetu.

Maisha ya Kristo yalionyesha mara moja na kwa yote kwamba Mungu hapendezwi na upatanisho unaotegemea utulizo wa kisheria; ambapo mtu

lazima afe ili kulipia deni ya dhambi ambayo Mungu aliagiza ilipwe – kwamba hadi kifo hiki kimetimizwa, na hasira ya Mungu kutulizwa. Hawezi samehe. Na maanisha ukweli? Haiwezi kuwa hivyo! Lina maantiki unapowaza kulihusu!

Maisha ya Kristo yanatuonyesha kwamba Baba anatamani tujue rehema yake, na kuwa kwake tayari kutusamehe dhambi zetu na kurejesha umoja wetu … UMOJA wetu … hiyo ndio sababu neno hilo “upatanisho” lilianzishwa.

Upatanisho … kuleta pamoja makundi mawili kuwa kitu kimoja.

Tulipokuwa tungali wenye dhambi, tulipokuwa tungali na ufahamu wa uongo kabisa wa tabia ya Mungu, Kristo alitufilia. Ni jinsi gani hilo lililo nzuri! Ni jinsi gani hilo lililo la rehema! Alikufa, sio kulipa deni ambalo Mungu alidai, bali kutuonyesha kwamba kiasili sisi ni wenye chuki na kuhukumu na wasioamini tabia ya kweli ya Mungu. Akiwa ametuonyesha jinsi tulivyo, wakati huo angesema, ‘Umetambua kwamba bado nakupenda? Bado nakupenda … haijalishi ulichokifanya au unachokifanya kwangu. Bado nakupenda … bado na kupenda!’

Hili ndilo hawakuelewa Mbinguni, pale mwanzo wa uasi wa Shetani. Malaika lazima waliuliza swali: upendo wa Mungu hutenda kazi namna gani? Hawakufahamu! Mbona Lusifa alikuwa ameondoka mbinguni? Alikuwa na sababu yoyote halali?

Umekuwa mchakato tata, kujifunza kuhusu upendo wa Mungu wa Agape. Umekuwa mchakato tata kwetu kuja kuelewa … kulinganisha Andiko na Andiko, na kushiriki mawazo yetu kuyahusu pamoja, na kuzuka na Injili hii ya kupendeza …. Sio kuzuka … kupokea INJILI HII TUKUFU. Mungu amekuwa akisubiria kwa maelfu ya miaka, akitarajia kwamba wanadamu wataufikia ukweli kuhusu upendo wake. Amekuwa akisihi kwamba tupokee ukweli kumhusu kama unavyodhihirikwa kupitia kwa Mwanawe. Kuna mtu yeyote ambaye anautaka? … Kuna yeyote ambaye anataka kuamini ukweli kumhusu? Ni bure! Yeyote? Ni bure! [… Anatusubiri tupokee hazina hii …] kununua bila pesa, bila gharama. Ndio, Kristo alitufilia. Mungu aliruhusu hili litendeke. Hakuamrisha kwamba lazima litendeke.

Kifo cha Kristo kwa mara moja na  ya mwisho kilituonyesha kwamba fikara zetu za upuuzi, kwamba mtu lazima afe ili kulipia dhambi, ni za kigeni kwake. Mungu alitoa kile ambacho kilikuwa cha thamani kuu kwake ili kamwe tusifikirie kumtuliza kwa chochote tena, kwa sababu ni ambacho kingemtuliza zaidi ya kile yeye mwenyewe alikuwa ametoa? Anatusihi akisema "hamuoni? Mimi ndiye nawapa na kuwapa; hamna chochote cha kunipa na sihitaji chochote ili kuponya uhusiano wetu!"

Ni nini tumejifunza hivi karibuni kuhusiana na wazo hili? Ni dhana ya kipagani. Kuamini kwamba lazima mtu angekufa ili kumlipa Mungu hasira yake ni dhana ya kipagani. Utulizo ni msingi wa upagani. Inahuzunisha kweli kwamba tumeshikilia dhana hii ya kipagani, na kuiita injili. Tumsifu Mungu kwa wingi wa rehema zake na msamaha wake!

Nini kilifanyika kwa Yesu siku tatu baada ya kifo chake msalabani? Yesu alifufuka. Sasa waza kuhusu hili kwa dakika! Kama adhabu ya dhambi ni utengano wa milele na Mungu kupitia kwa mauti, basi Yesu alikosa kutimiza hukumu. Kwa sababu hakufa milele. Watu wamekuwa katika ukosefu wa fahamu kwa siku nyingi kuliko zile ambazo Yesu alikufa … kwa hivyo haiwezi kuwa ni adhabu … haiwezi kuwa ilikuwa penalti.

Kama adhabu ya dhambi ni kumwaga damu, basi watu wengi wamemwaga damu yao katika historia na wengi wamemwaga damu kwa Mungu. Hivyo hawangekuwa wamelipa penalty yao wenyewe? lakini Wakristo watasema, "hapana, lazima ingekuwa ni damu takatifu …. Lazima ingekuwa ni damu *takatifu* kulipa adhabu ya sheria *takatifu* na ndio maana ni Kristo tu angefanya hivyo."

Katika hatua hii wakanamungu hurusha mikono kwa kufadhaika na kusema, "Mungu wako ni mwenye wazimu! Mungu wako anaagiza kifo cha Mwanawe mwenyewe kabla ya kuwasamehe wengine? Hiyo ni moja ya kichwa kigumu?" na nimejifunza na mkanamungu ambaye amedhihirisha wazo hili hasa. Kamwe hangekubali Mungu wa aina hiyo … lakini sasa anao uhusiano mzuri naye kwa sababu ya Injili yangu ya Milele, sio utulizo wa injili ya Mungu mwenye kiu ya damu.

Umati: Amina.

Sio kifo cha Mwanawe kilihitajika ili kulipia dhambi zetu. Mungu anataka kutusamehe tu. Anataka tu tuthamini jinsi tulivyo – Ungama. "Kama tukiziungama dhambi zetu, Bibilia inasema nini? "…Yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha toka kwenye udhalimu wote." (1 Yohana 1:9) Hilo tu ndilo anahitaji! Tujinyenyekeze, kutambua dhambi zetu, na kuja mbele zake kwa unyenyekevu.

Mungu anataka kutusamehe tu, lakini tunazidi kuweka masharti ambayo tunadhani kwamba anahitaji ili kutusamehe. Hilo sio jambo la ajabu? Na tunafanya hivyo kwa sababu hivyo ndivyo tunakabiliana sisi kwa sisi, na kwa hivyo tunafikiria kuna mantiki kwamba ndivyo Mungu lazima atakabiliana nasi. Hapana!

Kwa hivyo, kurejelea tu kabla ya kuingia katika sehemu ya mwisho ya mazungumzo:

1. Kwa sababu dhambi ilitutenganisha na Mungu katika Bustani ya Edeni, na ufahamu wetu potovu ulitufanya kumkimbia, Mungu alikasirika sana au kuhuzunishwa. Kwa hivyo mchakato wa upatanisho lazima ungewekwa. Injili ya milele ilianza katika Bustani ya Edeni.

2. Mawasiliano yote na wanadamu kuanzia hapo yalikuwa kupitia kwa Mwanawe, ambaye angezungumza na Adamu na Hawa katika Bustani, na kisha kupitia kwa Wazee na Manabii kadri wakati ulivyosonga, walipomruhusu kuja karibu nao. Angeweka mpango wa wokovu, lakini haukufahamika vyema wakati wote.

3. Mungu alimuagiza Musa kufanya Patakatifu ili akae miongoni mwao … kuwa karibu nao, wanawe. Utukufu wake ungedhihirisha wakati uwepo wake ulikuwa pamoja nao. La kuhuzunisha bila shaka hili lilikuwa na mipaka yake. Watu bado walienda kuitafuta miungu mingine ambayo ilitenda zaidi kama sisi.

4. Kwa hivyo Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee: na Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwake mwenyewe katika tendo la kupendeza, katika kila mguzo na uponyaji wa mtu; katika kuuvunja mkate na samaki na kuwalisha watu; kila mguso, kuwaguza wenye ukoma na kuitawadha miguu ya wanafunzi jioni ya mwisho; kuuvunja mkate na kikombe cha divai; kila tendo nzuri dogo lilitendwa kwa heshima na neema, na lilikuwa onyesho la tabia tukufu ya Baba. Lakini la kuhuzunisha, wengi walimkataa. “Alikuja kwa walio Wake,” Yohana anakumbuka, “lakini wao hawakumpokea.” (Yohana 1:11) Kwa kumkataa Kristo, walimkataa Baba tena.

Akijua upendo wa Baba yake kwetu, na njia ya kweli ya wokovu, Yesu aliorodhesha kwa ufupi kinachohitajika kwa upatanisho kati yetu na Baba yake. Wale ambao watapokea neno lake na kuamini ahadi yake, kwamba Mungu aliwapenda, watarejeshwa kwa ushirika na Baba, na Kristo mwenyewe.

Yesu alisema katika Yohana 14:23 – “Mtu yeyote akinipenda atalishika Neno Langu (ambalo ni neno la Baba) na Baba Yangu atampenda, **Nasi** tutakuja kwake na kufanya makao Yetu kwake.” Hiyo si ni ahadi ya kupendeza! Upatanisho utatendeka.

Na Yohana anachukua wazo hilo tena katika barua yake mwenyewe, katika 1 Yohana 1: 3-4. “Lile tuliloliona na kulisikia (katika fungu la 1 na 2 anazungumza kuhusu jinsi mikono yetu imeguza na kushika Neno la uzima), Twawatangazia, ili kwamba nanyi mwe na ushirika nasi (ushirika ni nini? Ni kuja pamoja, ni umoja, ni ukaribu, ni kuunganika kwa watu): ili kwamba nanyi muwe na ushirika nasi: ushirika wetu hasa ni pamoja na Baba na Mwanawe Yesu Kristo.”

Hivyo ndivyo ilivyo kwetu? Hicho ndicho tunawapa watu? Kuja ushiriki nasi … kwa kweli ushirika wetu ni pamoja naye Baba na pamoja na Mwanawe. Nini unaweza hitaji zaidi?

Vitu haswa ambavyo Yesu aliahidi Yohana alithibitisha alikuwa anashuhudia pamoja na waumini wenzake. Ndio, hiyo ndio tumeshuhudia pia … na ninafurahia kuwa na uiano na aina hiyo ya uhusiano, na aina hiyo ya upatanisho … na bila kutegemea mtu mwingine kutekeleza jukumu, na nimetaja hili awali, kutimiza jukumu ambalo Yesu na Baba yake hawawezi timiza tena kwa sababu bado wametenganishwa nasi. Upatanisho haumaanishi chochote bado wako kule nje na mtu mwingine tofauti lazima wachukue pahali pao.

Napenda ushirika ambao Yohana anarekodi! Ushirika pamoja na Baba na Mwana!

"Tunaandika mambo haya ili furaha yako ipate kuwa…" nusu timilifu? ... Hapana! … "Timilifu." Unaweza kuwa na utimilifu wa furaha pamoja na Baba na Mwanawe, kulingana na Maandiko.

"Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina Lake:" (Yohana 1:12)

Mhuri wa uwana wao ulikuwa Uwepo wa Roho wa Mwana: "Kwa sababu ninyi ni watoto wa Mungu, Mungu amemtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, anayelia, "Abbaa! Yaani, Baba." (Wagalatia 4:6)

Kwa hivyo tunapoamini kwamba Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtuma Mwanawe wa pekee, na tunapoamini kwamba Mungu alitupenda hata akamtuma Mwanawe wa pekee katika mioyo yetu, akilia Abbaa! Yaani Baba, na tutakapoamini kwamba kwa kweli tunaushirika na Baba pamoja na Mwanawe, kama tulivyoahidiwa na Yesu na kuthibitishwa na Yohana na kushuhudiwa naye, basi tunaweza jua kwa hakika kwamba mchakato wa upatanisho umekamilishwa ambao Mungu aliweka katika Bustani ya Edeni miaka 6000 iliyopita, akisubiria utekelezwe … na ambao unapatikana kwetu leo.

Leo maneno haya yametimizwa kwenye masikio yako. Mungu, kupitia kwa Mwanawe, Yesu Kristo. Amejiwasilisha yeye mwenyewe kwa uhusiano mzuri nawe, na mimi, na mtu yeyote mwingine kule nje ambaye atadai ahadi yake, kuukumbatia, na kuushikilia, ndio, na yeyote ambaye anautaka. Katika

uhusiano huu mzuri, Mungu anataka kukaa mioyoni mwetu, pamoja na Mwanawe, kupitia kwa Uwepo wake binafsi uitwao Roho Mtakatifu.

Sasa, Mungu alikuwa katika Patakatifu na hakuzunguka sana. Kisha alikuwa ndani ya Yesu, na aliweza kuzunguka Yerusalemu na sehemu zilizoizunguka, ikiwemo baadhi ya sehemu za watu wa mataifa. Lakini sasa ahadi imepanuliwa hadi Australia, New Zealand, Asia, Amerika, Afrika na kila mahali ambapo pana muumini ambaye anataka ushirika pamoja na Baba na Mwana. Kupitia kwa mchakato wa upatanisho, Baba anaweza kuweko nasi yeye mwenyewe. Na sasa ni umbali upi ambao Baba anaweza enea sasa? Ni wangapi wa wanawe ambao anauwezo wa kushiriki nao sasa?

Umati: Wote!

Wote … kupitia kwa Roho Mtakatifu. Tazama mchakato wa upatanisho ukienea kote … mapenzi ya Mungu yametimizwa! Katika Patakatifu, Mungu aliweza kuwa ***kati*** yao. Katika Kristo, aliweza ***kuwa*** nao. Na sasa, kupitia kwa Roho Mtakatifu, anaweza kuwa ***ndani*** yetu. Kwa kweli upatanisho umetimilika! Tumepatanishwa na Baba yetu wa Mbinguni. Halleluya.

## Vitu najisi hututenganisha na Mungu

2 Wakorintho 6:16-18

Kuna mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa kuwa sisi tu hekalu la Mungu aliye hai. Kama Mungu alivyosema: Nitakaa pamoja nao na kutembea katikati yao, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Kwa hiyo tokeni miongoni mwao, mkatengwe nao, asema Bwana. Msiguse kitu cho chote **kilicho najisi**, Nami nitawakaribisha. Mimi nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa wanangu na binti zangu, asema Bwana Mwenyezi.

Ni kitu gani **najisi** ambacho hututenganisha na Mungu? Ni kipande cha kuni ambacho kimechongwa au udongo ambao umefinyangwa kwa umbo la sanamu fulani? Hicho ndicho kitu najisi ambacho kitatutenganisha na

Mungu?  Ni sehemu ya chakula fulani ambacho sio kizuri kwa miili yetu? Hicho ndicho kitu najisi ambacho kitatutenganisha na Mungu? Ni kinywaji cha kulevya, chenye athari hasi kwenye akili na maamuzi? Vipi kuhusu mahali ambapo watu wabaya huenda na kufanya vitu vibaya? Pengine vitu hivi vyote ni najisi, na vinaweza tutenganisha na Mungu, lakini ni nini KITU HALISI ambacho hututenganisha na Mungu?

Umati: Vazi la Kibabeli.

Vazi la Kibabeli!

Umati: Utambulisho potofu.

Pengine kitu najisi kweli ambacho hututenganisha na Mungu ni kumfahamu visivyo na kumwasilisha visivyo kwa Baba yetu wa Mbinguni: kumhukumu Mungu vibaya kwa kumfanya kuwa Mungu mwenye hasira, kisasi na kuchukia, na sivyo alivyo! Labda haya ndio mawazo najisi ambayo hututenganisha na Mungu? Kutoka kwa ufahamu wetu najisi wa Mungu kunatokea matendo yote najisi na mawazo kuelekea kwa Mungu; na ukosefu wa muunganiko hufanya utiifu wetu kukosa tumaini. Picha hii potovu ya Mungu imeweka kizuizi najisi kwa mioyo yetu.

Mruhusu akiondoe kwa ufunuo wa upendo wake unaopatikana kwa Mwanawe, Yesu Kristo. na umruhusu akupokee unapoacha kumkimbia.

Ukimruhusu kurejea moyoni mwako, kama ilivyo hamu yake, tena, kwa ruhusa yako, atakuwa Baba kwako, na tutakuwa wana na binti zake.

Mkaribieni Mungu, naye bila shaka hufanya nini?

Umati: Hutukaribia.

Ndio, Hutukaribia! (Yakobo 4:8) hicho ndicho ametaka daima. Lakini hutuongojea tuipokee Roho wake. Huu umekuwa mpango na hamu yake kwa muda mrefu … kwamba tunaweza mruhusu aingie.

Wakati ambao habari hii ya ufalme itahubiriwa ulimwenguni kote, kama ushuhudu kwa mataifa yote, basi mwisho utakuja. Kisha kutembea kwetu na Mungu kusichoonekana na Mungu wetu sasa kutapisha kutembea na Mungu wetu kunakoonekana Yesu atakaporejea na kutupeleka nyumbani kwa nyumba ya Babake, ambapo makao yameandaliwa na kutusubiria … kwa muda mrefu.

Ni hamu yako kuwa pamoja naye alipo?

Ni hamu yako kuwa alipo?

Umati: Ndio!

Basi mruhusu awe ambapo anataka kuwa sasa hivi!

Umati: Amina!

Mruhusu awe ambapo anataka kuwa sasa hivi. Huo ni upatanisho … kuwa karibu nawe zaidi: kwa kweli, moyoni mwako … hiyo ndio hamu yake. hivi karibuni, na karibuni sana tutarejeshwa nyumbani kwetu mbinguni na hatutatenganishwa tena.

Tupeleke habari hii njema kwa ulimwengu wote, na tuache watu wote wajue kwamba Baba yao wa mbinguni hana nia mbaya nao. Wacha watu wajue kwamba anatamani kupatanishwa nao na kuchukua pahali katika mioyo yao vilevile, na kuwapa mwisho unaotarajiwa … mwisho mzuri … mwisho wa kupendeza. Ulimwengu unahitaji habari njema sasa hivi, sivyo?

Umati: Ndio!

Wacha tuwe ambao wanaipeana. Wacha tuipokee na kushiriki kile ambacho tumeshuhudia … tulichokiona, na kusikia, na kuhisi, na kukiguza kwa mikono yetu wenyewe na kubeba.

Mungu atubariki tunaposhiriki, sio kile tunajua tu, bali kile ambacho tumeshuhudia na tunaendelea kushuhudia pamoja na Baba yetu, na Mwanawe, pamoja na watu wote ulimwenguni. Wacha tuwaonyesha

kwamba kuna Mungu katika Israeli ambaye anatamani kumtuma Mwanawe kuturejesha nyumbani kuwa naye. Amina!

Umati: Amina!

Wacha tuombe: Baba yetu mwingi wa neema, tunakushukuru kwa uwazi wa ujumbe wa Maandiko, kwamba sio wewe umeweka kizuizi kwetu, bali ni sisi tumeweka kizuizi kwako. Tusamehe, Baba, kwa hili. Tusamehe kwa kukosa kukufahamu, kwa kukufikiria kuwa kitu kisicho sahihi kabisa.

Tunakushukuru kwa sababu umetufuata. Ulimtuma Yesu ulimwenguni kuja na kutafuta na kuokoa kilichopotea. Ulikuwa ndani yake ukiupatanisha ulimwengu kwa nafsi yako mwenyewe. Umetupa Neno la upatanisho; umetupa nafsi yako mwenyewe, Roho wako, ikae ndani yetu, kutenda kazi yako njema ndani yetu.

Baba tunapoondoka kutoka kwa kambi hii, jioni ya leo au kesho, tunapotengana, mioyo yetu itahuzunika kwa sababu tunapendana hapa; tunafurahia uwepo na ushirika wa kila mmoja, utimilifu wa furaha, ila, lazima twende. Kuna kazima ya kufanya mahali mbalimbali, naomba mibaraka yako iende na kila kichwa ambacho kimeinamishwa hapa, na kila mmoja na familia ambayo inatazama kwenye mtandao. Baba, wabarika na uhakikisho kwamba Mungu anawapenda kwa vyovyote vile na tunaweza acha kujipiga kwa hukumu ya nafsi na adhabu, kwa sababu hukumu yako ndio mwisho, na utatupa kile ambacho tunatamani.

Baba, naomba kwamba mapenzi yako yawe mapenzi yetu. Kwamba kusamehe kwako na kuwa tayari kusamehe kuakisiwe katika kuwa tayari kwetu kusema samahani na kugeuka kutoka kwa dhambi zetu, ili uwezi kutimiliza kazi yako njema ili maisha ya Kristo na nia ya Kristo iwe nia yetu.

Baba nakushukuru tena kwa sababu ya ujumbe wote wa juma hili, ujumbe wa kupendeza ambao umetoka hapa mbele. Nakushukuru kwa sababu tunaweza rekodi na kuweka kwenye mtandao ili watu watazame, kwa sababu kama sauti zetu zitakimia, Neno lako litaendelea.

Bariki neno lako, Bibilia, katika kila pembe ya dunia. Ambapo watu wanaisoma, watambue Ukweli kama ulivyo katika Kristo, ili kazi yako, na utukufu wa Mungu miongoni mwa mataifa yote, itakamilika na mwisho uje. Nakushukuru Bwana kwa kulisikia ombi hili, pamoja na wakati huu katika jina la Yesu … Amina.

Kikao cha jioni kando ya moto wa kambi huhisika kuwa kizuri. Na kama mtu ambaye haupendi yuko pale? Saa hizo chache zitakuwa za wasiwasi kwa wahusika wote.

Sasa fikiria kukaribishwa kuishi milele katika moto wa kambi ya Mungu mbinguni. Lakini umesikia mambo mengi mabaya kumhusu... mbona utake kukaa milele na mtu mwenye kudhibiti na mwenye hasira, mtu ambaye haumpendi? Vizuri, hiyo ni hitimisho yako kumhusu Mungu kutokana na kile ambacho umesikia kutoka kwa Wakristo na wasio-Wakristo sawia.

Na lakini kama sote tumedanganywa? Na kama sio mthibiti mkaidi jinsi watu wamemfanya kuwa? Na kama yeye ni Baba ambaye kwa kweli anawatakia wanawe mema tu, anataka kuwa karibu nao? Anawezaje badilisha mtazamo wetu potovu na kuweka ndani yetu hamu yakuwa nyumbani na Baba? Tazama Baba yetu wa Mbinguni anapojaribu kuweka vitu sawa kwa ajili yetu, akitarajia tutabadilisha mawazo yetu kumhusu. Kamwe hajabadilisha mawazo yake kutuhusu.